- Kuungua kwa sukari (starch) kwenye jani wakati wa kukausha lamina na migongo (lamina and stem drying). Hitilafu hiyo hutambulishwa kwa herufi “K” kwenye uteuzi.
- Mmea kushindwa kuchuja mbolea vizuri – Hitilafu hiyo huathiri majani ya tumbaku ikiwa mmea hautapata maji (moisture) ya kutosha kuwezesha mbolea/virutubisho vilivyonyonywa na mmea kutotumika kwenye mwili wa mmea. Hitilafu hiyo husababisha majani kuwa magumu na mazito kama ngozi na hutambulishwa kwa herufi “KD” kwenye uteuzi.
- Kijani kigumu (hard green). Hii hutokana na kuvuna majani machanga ambayo hayajakoma na majani yaliyochubuliwa wakati wa uvunaji au kuachwa juani. Mkulima anashauriwa kuvuna majani yaliyokoamaa vizuri na kuzingatia ubebaji na utunzaji kabla ya kukaushwa. Kijani hicho hujitokeza kwenye lamina na hakifutiki na hutambulishwa kwa herufi “G”.
- Kinyevu (water stain) – hitilafu hii hutokea wakati wa ukaushaji katika hatua ya kukausha jani. Mkulima hutakiwa kufungua madirisha ya juu ili kuwezesha maji yaliyopo kwenye jani kutoka nje. Ikitokea mkulima amechelewa kufungua madirisha husababisha maji hayo kuchirizika kwenye majani na kuweka alama kama jasho na kuharibu rangi ya jani (discoloration) na kuvuta kinyevu (waterstain).

## WASILIANA NASI:


**Mkurugenzi Mkuu,**
**Bodi ya Tumbaku Tanzania,**
**5 Barabara ya Kihonda Maghorofani - Bima,**
**S.L.P 227,**
**67128 Morogoro.**
**Tovuti: www.tobaccoboard.go.tz**
**Barua pepe: info@tobaccoboard.go.tz**


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA KILIMO**

**BODI YA TUMBAKU TANZANIA**

# UKAUSHAJI WA TUMBAKU

## Utangulizi

Hatua ya ukaushaji ni ya muhimu sana katika kilimo cha tumbaku. Kwa ukaushaji mzuri wa tumbaku, bani la kukaushia tumbaku linapaswa kuwa na madirisha madogo kwa ajili ya kuruhusu kusambaa kwa joto na unyevunyevu unaohitajika kwenye bani. Hewa ya nje kwa kawaida huingia ndani ya bani kupitia madirisha hayo madogo yaliyopo chini na juu. Joto linalozalishwa kuanzia kwenye jiko husambaa kwenye bani zima kupitia bomba zinazosafirisha joto

## Mambo ya msingi ya kuzingatia wakati wa ukaushaji wa tumbaku kwa njia ya mvuke

1. Bani imara lenye uwezo wa kutunza joto na kuwa na mzunguko mzuri wa hewa.
2. Jani lenye uwiano mzuri wa kiwango cha Nitrojeni na wanga.
3. Jani la tumbaku lililokamaa vizuri .
4. Uelewa mzuri wa mkulima juu ya hatua za ukaushaji wa jani la tumbaku.
5. Hali nzuri ya hewa.

## Mazingira ya ukaushaji yanatawaliwa na mambo makuu matatu:-

- i. Hali ya hewa ya joto ya ndani ya bani
- ii. Hali ya Mzunguko wa hewa ndani ya bani
- iii. Hali ya unyevunyevu ndani ya bani

## Hatua za ukaushaji wa jani la tumbaku ndani ya bani

- i. Kubadili jani kuwa la njano (Yellowing) kiasi cha joto kinachotakiwa ni 90 - 105ºF kwa muda wa masaa 30 - 60. Madirisha madogo yote yafungwe.
- ii. Uwekaji wa rangi (Fixing colour) kiasi cha joto kinachotakiwa ni 105 - 125ºF kwa muda wa masaa 26 - 40. Madirisha madogo yote yafunguliwe nusu.
- iii. Ukaushaji wa jani (Lamina drying) kiasi cha joto kinachotakiwa ni 125 - 140ºF kwa muda wa masaa 10 - 16. Madirisha madogo yote yafunguliwe nusu.
- iv. Ukaushaji wa migongo ya jani (midrib drying) kiasi cha joto kinachotakiwa ni 140 - 160ºF kwa muda wa masaa 20 - 32 Madirisha madogo yote yafunguliwe.

## Kuchambua na Kupanga Tumbaku

Mkulima baada ya kukausha tumbaku yake anatakiwa kuchambua na kuipanga kwa kuzingatia jinsi inavyofanana.

Mambo ya kuzingatia katika uchambuzi na upangaji wa majani ya tumbaku

- a. Mchumo - Hii ni nafasi ya jani katika mmea yaani majani ya chini, kati na juu.
- b. Ubora wa majani - Hali ya usafi wa jani
- c. Rangi- majani ya tumbaku baada ya kukaushwa WASILIANA NASI:wa na rangi tatu ambazo ni Chungwa, Limao na Kahawia (mahogany)
- d. Urefu - majani yenye urefu sawa huwekwa kwenye kundi moja
- e. Hitilafu (Factors) - majani ya tumbaku yanaweza kupata hitilafu mbalimbali wakati wa ukaushaji au kabla ya kuvunwa. Hitilafu hizo zinaweza kuwa kuungua kwa sukari, kuwa na kijani chepesi au kigumu, kuwa na unyevu zaidi yTa asilimia 14 na usiozidi asilimia 16

Tumbaku baada ya kuchambuliwa na kupangwa kwa kuzingatia kufanana kwake hufungwa kwenye vishada na baadaye hufungwa kwenye mabelo. Belo moja linatakiwa kuwa na tumbaku inayofanana ambayo ni daraja moja.

## Uteuzi wa Tumbaku

Tumbaku hupewa madaraja kabla ya kununuliwa. Kitendo cha kutoa daraja kwenye tumbaku huitwa Uteuzi (Classification). Mteuzi kutoka Bodi ya Tumbaku huteua tumbaku ikiwa sokoni.

## Misingi ya uteuzi wa tumbaku

- i. Michumo (plant position) - Hii ni nafasi ya jani kwenye mmea. Michumo inayotambulika ni Primings, Lugs, Cutters, Smoking leaf, Leaf na Tips. (Primings na Lugs hutumia herufi X, Cutters C, Smoking leaf, Leaf na Tips L).
- ii. Ubora - Hupimwa kwa hali ya usafi au kuchakaa kwa jani. (1, 2, 3, 4, 5). Majani yenye uharibifu asilimia 1 hadi 5 ni 1, asilimia 6 hadi 10 ni 2, asilimia 11 hadi 15 ni 3, asilimia 16 hadi 20 ni 4, asilimia 21 hadi 25 ni 5, asilimia 26 hadi 30 ni nondescript 1 na asilimia 31 hadi 40 ni nondescript 2.
- iii. Rangi - majani ya tumbaku huweza kuwa na mojawapo ya rangi hizi tatu chungwa (orange), Limao (lemon) au kahawia (mahogany). Katika uteuzi chungwa hutambulika kwa herufi "O", Limao "L" na Kahawia "R".
- iv. Hitilafu (factors) - katika utunzaji wa tumbaku kuanzia shambani hadi kwenye maghala, majani ya tumbaku yanaweza kupata hitilafu. Hitilafu hizo hupunguza ubora wa zao. Katika uteuzi hitilafu zifuatazo huzingatiwa.

  - Kijani chepesi (running green); hii hutokea kwenye bani wakati wa kuweka rangi (color fixing), mkulima akipandisha joto mapema kabla ya kukamilika vyema kwa kubadilika kwa rangi. Rangi ya kijani chepesi kwenye migongo ya jani yaani midrib. Hitilafu hii hutambulika kwa herufi "V"